Hospitali Iliyothibitishwa kwa ISO 9001: 2015

# HOSPITALI YA MAFUNZO NA RUFAA YA MOI

## SERA YA FARAGHA YA DATA

MTRH imesajiliwa kama **Mdhibiti na Mchakataji wa Data**. Afisa wa Ulinzi wa Data na Naibu Afisa wa Ulinzi wa Data wameteuliwa kusimamia na kuhakikisha Sheria ya Ulinzi wa Data ya mwaka 2019 inafuatwa. Maelezo ya mawasiliano yao ni kama ifuatavyo;

| | |
|---|---|
| 1. Ms. Margaret C. Koech<br>Afisa wa Ulinzi wa Data<br>S.L.P 3-30100,<br>Eldoret.<br>Barua pepe: dpo@mtrh.go.ke | 2. Mr. Moses K. Mbiti<br>Naibu Afisa wa Ulinzi wa Data<br>S.L.P 3-30100,<br>Eldoret.<br>Barua pepe: ddpo@mtrh.go.ke |

### 1. TAMKO LA FARAGHA

Tamko hili la faragha linaeleza jinsi tunavyokusanya, kutumia, kuchakata na kulinda taarifa zako binafsi kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Data ya mwaka 2019 na kanuni zake.

Tamko ili linapaswa kusomwa pamoja na Sheria na Masharti ya Matumizi ya huduma zingine zinazotolewa na MTRH. Iwapo kutakuwa na mgogoro kuhusiana na faragha ya data, tamko ili la faragha ndilo litakalotumika.

Tamko ili linawahusu wagonjwa wote, wafanyakazi, wanafunzi, wasambazaji, washauri, wahusika wa tatu, mashirika ya umma (parastatal), washirika wa kimaendeleo pamoja na wageni wote wa MTRH.

### 2. UFANUZI WA MANENO

"MTRH" Inamaanisha Moi Teaching and Referral Hospital lililoanzishwa kwa kuchapishwa notisi ya Kisheria No. 78 wa 1998 Kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma (State Corporations Act), Sura ya Sheria (CAP) 446 Sheria ya Kenya.

**"Afisa wa Ulinzi wa Data"** ni mtu aliyeteuliwa au kuteuliwa na MTRH kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Data, Na. 24 ya mwaka 2019 na Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hiyo.

**"Ukusanyaji wa Data"** unamaanisha kukusanya taarifa zinazokuhusu.

**"Data binafsi"** ni taarifa zinazokuhusu ambazo zinakutambulisha moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kama mtu wa kipekee, kama vile jina, namba ya utambulisho, taarifa za mahali ulipo, kitambulisho cha mtandaoni au sifa moja au zaidi mahususi za kimwili, kifiziolojia, kijeni, kiakili, kiuchumi, kitamaduni au kijamii zinazomtambulisha mtu halisi.

"**Uchakataji**" unamaanisha kitendo au Kundi la vitendo vinavyofanywa kwa data zako binafsi, iwe kwa njia za kiotomatiki kama vile: ukusanyaji, kurekodi, kupanga au kimiundo; kuhifadhi, kurekebisha au kubadilisha; kupata tena, kushauri au kutumia; kufichua, kwa namna nyingine yoyote kufanya zipatikane; kufungamanisha au kuunganisha, kuweka mipaka, kufuta au kuharibu.

"**Data binafsi nyeti**" ni data inayoonyesha asili yako ya kikabila au rangi, maoni ya kisiasa, uanachama wa kitaaluma, pamoja na uchakataji wa data za kijeni, data za bayometriki kwa madhumuni ya kumtambulisha mtu halisi, data zinazohusu afya au data zinazohusu jinsia ya mtu halisi.

"**Mhusika wa Tatu**" unamaanisha mtu halisi au Kundi/vikundivilivyobuniwa kisheria, mamlaka ya umma, shirika au taasisi nyingine isipokuwa wewe na MTRH, ambaye chini ya mamlaka ya moja kwa moja ya **MTRH** anaidhinishwa kuchakata data zako binafsi.

## 3. MSINGI WA KISHERIA

**MTRH** itachakata data zako binafsi kulingana na sheria zinazotumika:

1. Kwa idhini yako.
2. Wakati uchakataji unahitajika kutekeleza jukumu la Mamlaka.
3. Kwa ajili ya utekelezaji wa mkataba ambao wewe ni mdau au kwa ombi lako kabla ya kufanya mkataba.
4. Kwa uzingatiaji wa wajibu wowote wa kisheria ambalo **MTRH** inakubaliana nalo.
5. Kwa ajili ya kulinda maslahi muhimu na halali ya **MTRH** au mtu mwingine.
6. Kwa ajili ya utekelezaji wa jukumu linalofanywa kwa maslahi ya umma.
7. Kwa ajili ya utafiti wa kihistoria, takwimu, au kisayansi.

### 3.1 Ukusanyaji wa Data Binafsi

MTRH inakusanya data zako binafsi moja kwa moja na kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa mujibu wa sheria. Tunakusanya taarifa zako binafsi kwa ufahamu na idhini yako, isipokuwa katika hali ambapo idhini kabla ya ukusanyaji haiwezi kupatikana kwa sababu halisi na uchakataji wa data unaruhusiwa kisheria.

Tunaweza kukusanya taarifa binafsi kutoka kwako, kama vile jina lako, barua pepe, nambari ya simu, na taarifa nyingine yoyote binafsi unayochagua kutupatia. Pia tunaweza kukusanya taarifa zisizo binafsi, kama vile anwani yako ya IP na program kivinjari, kupitia vidakuzi au teknolojia za kufuatilia kama vidakuzi baada ya kupeana idhini yako unapokubali vidakuzi.

Wakati wa kutoa huduma kwako, pia tunaweza kukusanya data nyeti zinazolingana na kanuni, kama vile zile zilizo chini ya **Wizara ya Afya, Kenya** na mashirika mengine husika za serikali.

#### 3.1.1 Data Binafsi Nyeti

**MTRH** inakusanya aina maalumu ya data binafsi kukuhusu inayofichua taarifa kuhusu rangi yako, hali ya afya, asili ya kikabila, imani, mali yako, hali ya ndoa, taarifa za familia ikiwa ni pamoja na watoto, wazazi, mke/mume au wake, jinsia na data za bayometriki.
**MTRH** itahakikisha kwamba data binafsi nyeti kukuhusu inachakatwa kwa mujibu wa haki yako ya faragha kama inavyoruhusiwa katika Sehemu ya V ya Sheria ya Ulinzi wa Data, 2019.

3.2 Matumizi ya Data Binafsi

| Nambari | Wadau | Data binafsi inayokusanywa | Madhumuni |
|---|---|---|---|
| 1. | Wagonjwa | Jina, Namba ya Kitambulisho, Mtu wa Karibu, Nambari ya Simu, Kaunti ya makazi, Anwani, Tarehe ya Kuzaliwa, Jinsia | Kwa huduma na usimamizi wa kimatibabu |
| 2. | Wanafunzi | Jina, Nambari ya Kitambulisho, Jinsia, Mtu wa Karibu, Nambari ya Simu, Kaunti ya makazi, Anwani, Tarehe ya Kuzaliwa, majina ya wazazi/mlezi na maelezo ya mawasiliano | Kwa masuala ya elimu |
| 3. | Wafanyakazi | Jina, Anwani ya posta na ya makazi, Mahali ulipo, Nambari ya simu, Tarehe ya kuzaliwa, Barua pepe, Umri, Jinsia, Taarifa za wategemezi, Taarifa za kielimu, Kitaaluma, Data za bayometriki kama alama za vidole, Rekodi za CCTV, Rekodi za kiafya | Usimamizi wa ajira na mahusisno ya kikazi na uchakataji wa faida |
| 4. | Wategemezi wa wafanyakazi | Aina ya utambulisho, Jina, Anwani ya posta na ya makazi, eneo ulipo, Nambari ya simu, Tarehe ya kuzaliwa, Barua pepe, Umri, Jinsia | Uchakataji wa faida za wategemezi wa wafanyakazi |
| 5. | Wanagenzi/Wanafunzi wa mafunzo ya viwandani | Aina ya utambulisho, Jina, Anwani ya posta na ya makazi, eneo ulipo, Nambari ya simu, Tarehe na mahali pa kuzaliwa, Barua pepe, Umri, Jinsia, Taarifa za akaunti, Taarifa za familia – mtu wa karibu, Taarifa za kielimu, Kitaaluma, Rekodi za CCTV | Uchkataji wa uanagenzi na mafunzo ya viwandani |
| 6. | Watafiti | Aina ya utambulisho, Jina, Anwani ya posta na ya makazi, eneo ulipo, Nambari ya simu, Jina la Taasisi ya Elimu, Barua pepe, Rekodi za CCTV | Ualalishaji wa maombi |
| 7. | Washirika wa kimaendeleo / wawakilishi | Jina, Nambari ya simu, Barua pepe, Rekodi za CCTV, Washirika wa kimaendeleo waliohusiana | Usimamizi wa mahusiano na washirika wa kimaendeleo |
| 8. | Watu wengine / wahusika kama vile kampuni za bima, NSSF, Taasisi za kifedha, Makampuni ya sheria, Washauri, Wasambazaji, wazabuni n.k | Aina ya utambulisho, Jina, Anwani ya posta na ya makazi, eneo ulipo, Nambari ya simu, Tarehe ya kuzaliwa, Barua pepe, Umri, Jinsia, Taarifa za kielimu, Kitaaluma, Rekodi za CCTV | Utawala wa shughuli za ununuzi na mikataba |

### 3.3 Kufikia Data yako Binafsi

Ufikiaji wa data yako binafsi unazuiliwa kulingana na kanuni ya "sababu ya kutaka kujua" na kanuni ya "haki chache zilizothibitiwa". Tunachukua hatua kuhakikisha data zako binafsi hazibadilishwi na vyombo au watu wasioruhusiwa. Watu wote walioidhinishwa kufikia data zako binafsi kulingana na wajibu wa usiri.

#### 3.3.1 Haki Zako za Kisheria

Chini ya Sheria ya Ulinzi wa Data, 2019, una haki zifuatazo kuhusiana na data zako binafsi:
Haki ya:

i. Kupata taarifa (haki ya kufahamishwa)
ii. Kufikia data zako binafsi
iii. Kuomba kurekebishwa kwa data zako binafsi
iv. Kuomba kufutwa kwa data zako binafsi
v. Kupinga uchakataji wa data zako binafsi
vi. Kuweka mipaka ya uchakataji wa data zako binafsi
vii. Kuhamisha data zako binafsi
viii. Kuondoa idhini

Tafadhali wasiliana nasi unapohitaji kutumia haki zilizotajwa hapo juu.

### 3.4 Uhamishaji na Usambazaji wa Data Binafsi

#### 3.4.1 Usambazaji wa Data

MTRH itasambaza data zako binafsi kwa idhini yako na kwa njia inayolingana na madhumuni ambayo data ilikusanywa.

Tunaweza kusambaza au kufichua data binafsi tunayokusanya kwa wahusika wa tatu wanaotoa msaada kwa MTRH kufanikisha utoaji huduma. Pia, tutafichua au kuchakata data zako binafsi kwa mhusika wa tatu itakapohitajika kisheria.

Sera yetu ni kutumia wahusika wa tatu ambao wamewajibika kudumisha viwango vinavyofaa vya usalama na usiri, na kuchakata taarifa binafsi kama ilivyoagizwa na **MTRH**.

#### 3.4.2 Uhamishaji wa Data

Iwapo **MTRH** imepokea idhini kutoka kwa mhusika wa data, inaweza kuhamisha data binafsi kwenda mataifa mengine, wadau, washirika au taasisi nje ya Kenya kwa madhumuni kama utafiti, huduma za matibabu, ajira, elimu, n.k., mradi nchi hizo, wadau, washirika au taasisi zina sheria sawa za ulinzi wa data na zimearifu **Kamishna wa Data**.

Iwapo **MTRH** itapitia mabadiliko ya kibiashara, data zako binafsi zinaweza kuwa miongoni mwa mali zinazohamishwa kwenye majukwaa mapya au taasisi mpya, na mnunuzi wa mali za data anaweza kuendelea kuchakata data binafsi.

### 3.5 Ulinzi wa Data Binafsi

**MTRH** inahakikisha upatikanaji wa hifadhi za kielektroniki na za kimwili zenye data zako binafsi unadhibitiwa kwa kutumia taratibu za kiutawala, kimwili, na ulinzi kutoka kwa Shirika (MTRH).

Tumeweka hatua za kiusalama kulinda taarifa zako dhidi ya ufikiaji usioruhusiwa.

### 3.6 Uhifadhi wa Data Binafsi

Tutahifadhi data zako binafsi tu kwa ajili ya kutimiza madhumuni ya kukusanya data na kutimiza mahitaji yoyote ya kisheria tuliyo nayo. Ili kubaini muda sahihi wa uhifadhi, tunazingatia ukubwa, asili na unyeti wa data, madhumuni ya uchakataji, umuhimu wa kufuata sera za ndani, na mahitaji ya kisheria.

Kwa sababu ya asili ya jukumu letu, tunaweza kuhifadhi data zako binafsi kulingana na ratiba za Uhifadhi na Utupaji wa Rekodi za MTRH au wajibu mwingine wa kisheria.

Katika baadhi ya hali, unaweza kuomba kufuta data zako binafsi kulingana na haki zako za kisheria zilizotajwa katika kipengele 3.7.

## 4. MATUMIZI YA VIDAKUZI, PROGRAMU JALIZI ILIYOPACHIKWA, KIDIRISHA KIDOGO NA VIUNGO

Tovuti ya MTRH inatumia vidakuzi kukupatia matumizi ya kibinafsi na rahisi. Inatuwezesha kukutambua kila wakati unapoingia kwenye tovuti. kidakuzi ni faili la maandishi lililowekwa kwenye diski kuu yako na seva ya wavuti.

Taarifa zilizohifadhiwa kwenye kidakuzi zinaundwa na seva wakati unapoingia kwenye tovuti. Taarifa hii ina kitambulisho cha kipekee kwako na tarakilishi chako na inaweza kusomwa tu na seva ya wavuti katika kikoa iliyotoa kidakuzi.

**Kuondoa na Kuwezesha Vidakuzi**

Unaweza kubali au kukataa vidakuzi.
Unaweza kuondoa vidakuzi kupitia kiungo hiki:
www.mtrh.go.ke/delete-cookies

Pia unaweza kuondoa/kuwezesha vidakuzi kupitia kivinjari chako. Kizuizi kinaweza kuathiri kuzuru sehemu za tovuti yetu. Unaeza zuia vidakuzi kwa kuwezesha mipangilio kwenye kivinjari chako kitakacho kuruhusu kuondoa vidakuzi vyote au kadhaa. Hata hivyo ukitumia mpangilio wa kivinjari chako kuzuia vidakuzi vyote, unaeza kosa uwezo wa kuingia kwenye sehemu au tovuti nzima.

Hapa chini ni viungo vya maelekezo:

i. **Internet Explorer:** https://support.microsoft.com/fr-fr/help/17442
ii. **Mozilla Firefox:** https://support.mozilla.org/fr/kb/activer-desactiver-cookies
iii. **Safari:** https://support.apple.com/kb/PH21411?viewlocale=fr_FR&locale=fr_CA
iv. **Chrome:** https://support.google.com/accounts/answer/61416?hl=fr
v. **Opera:** http://help.opera.com/Windows/10.20/fr/cookies.html

Ndani ya tovuti, kuna Programu jalizi iliyopachikwa, Kidirisha kidogo na Viungo viungo kwa tovuti zisizo za mtrh (tovuti za Pamoja. Tovuti hizi zinafanya kazi kwa kujitegemea na zina sera zao za faragha. Unapoingia kwenye tovuti hizi inamaanisha umeondoka kwenye tovuti yetu na hautakua chini ya sera zetu za faragha na usalama. MTRH haijalazimika kwa sera za faragha au usalama wa tovuti zingine, wala haiidhinishi tovuti hizi au maudhui yao.

## 5. TATHMINI YA TAMKO LA FARAGHA

MTRH itatathmini Tamko la Faragha mara kwa mara au pale linapohitajika.

6. JINSI YA MAWASILIANO

MTRH inakaribisha maswali au maelezo kuhusu jinsi inavyochakata data zako binafsi, au iwapo unataka kutumia haki zako zinazohusiana na data binafsi. Tafadhali wasiliana nasi kwa Simu: :(+254)053-2033471/2/3/4 au kwa kutuandikia barua pepe kwenye: ceo@mtrh.go.ke na kwa nakala kwa dpo@mtrh.go.ke.

DKT. PHILIP K. KIRWA (MKURUGENZI MTENDAJI)

SAHIHI:..........................................................................................

TAREHE: 29/6/2026 ........................................................................................ 29 JUN 2026

MOI TEACHING AND REFERRAL HOSPITAL

P. O. BOX ...